



**HALMASHAURI YA MJI KASULU**  
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu: +255282810335  
Tovuti: [www.kasulutc.go.tz](http://www.kasulutc.go.tz)  
Baruapepe: [td@kasulutc.go.tz](mailto:td@kasulutc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji  
Halmashauri ya Mji Kasulu  
S. L. P 475  
KASULU.

KUMB NA. KSTC/S.1/20/79

09/08/2023

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kasulu anawatangazia watanzania wote wenye sifa na vigezo kutuma maombi ya nafasi ya kazi ya Mtendaji wa Mtaa III kwa kuzingatia sifa, vigezo na maelekezo yaliyo katika tangazo hili.

**1. Mtendaji wa Mtaa III (Nafasi 10)**

**Sifa za Mwombaji.**

- (i) Cheti cha Kidato cha IV au VI
- (ii) Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na sayansi ya sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.
- (iii) Awe hajawahi kuajiriwa Serikalini.

**Kazi za Kufanya:-**

1. Mratibu na Mtekelezaji wa sera na sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
2. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya Maendeleo katika Mtaa.
3. Msimamizi wa Utekelezaji wa sheria ndogo pamoja na sheria zinazotumika katika Mtaa.
4. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
5. Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa.
6. Kusimamia Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
7. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa.
8. Kusimamia Utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo ndogo za mitaa.
9. Na atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

NEW 9/8/2023

NEW

**MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mshahara kwa watumishi wa Umma TGS B<sub>1</sub>

**Masharti ya kazi.**

Kazi ina masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.

**MAMBO YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI.**

1. Muombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu.
2. Awe mwenye umri kati ya miaka 18 -45.
3. Barua za muombaji ziambatishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, Cheti cha Kuzaliwa na Picha mbili(2) za rangi (Passport size) za hivi karibuni.
4. Maomba ya kazi yaambatishwe na nakala ya kitambulisho cha nida au namba ya nida.
5. Barua za maombi ziambatishwe na maelezo binafsi ya muombaji (CV).
6. Testimonials, "Provisonal Results" Statement of Results" hati za matokeo za kidato cha Nne na sita (Form IV and Form VI Results Slips) **HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA)


**Namna ya Kuwasilisha maombi:-**

(i) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono.

(iii) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **22/08/2023** saa **9:30** Alasiri

**Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-**

Mkurugenzi wa Mji,  
Halmashauri ya Mji,  
S.L.P 475,  
KASULU.



**Julius K. Buberwa**  
Kaimu Mkurugenzi wa Mji  
Halmashauri ya Mji  
**KASULU**

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI  
KASULU